TARI
Transforming Agriculture

IFAD
INTERNATIONAL FUND FOR AGRICULTURAL DEVELPMENT

## TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA

# KILIMO BORA CHA ALIZETI




**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**
**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)**
**Kituo cha Ilonga**
**S.L.P 33, Kilosa, Tanzania**
**Simu: +255 736 623 283/759 703 615**
**Barua Pepe: cdilonga@tari.go.tz**
**Tovuti: www.tari.go.tz**



TOLEO 2025
Uchapishaji umegharamiwa na Mradi wa IFAD

## UTANGULIZI

Zao la alizeti ni miongoni mwa mazao ya mbegu za mafuta, zao hili hutoa mafuta ya kula kwa binadamu na mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo.

Alizeti ni zao lenye thamani kiuchumi na mafuta hutumika katika utengenezaji wa vipodozi, madawa na nishati mbadala kwenye viwanda

Maua ya alizeti hutumika kama mapambo na kutoa chavua kwa ajili ya nyuki kutengeneza asali

Ili kuongeza tija ya uzalishaji wa alizeti inashauriwa kufuata maelekezo ya kipeperushi hiki na mwongozo na kalenda ya kilimo bora cha alizeti uliotolewa na wizara ya Kilimo **mwaka 2022.**



Kichwa cha mbegu bora ya alizeti aina ya Record

## IKOLOJIA YA KILIMO CHA ALIZETI

Alizeti hustawi katika maeneo ya ikolojia tofauti

### Mwinuko

Zao la alizeti hustawi katika maeneo yenye mwinuko kati ya mita 0 - 2300 kutoka usawa wa bahari.

### Udongo

Alizeti hustawi kwenye udongo wenye kiwango cha uchachu (pH) kati ya 5.5 hadi 8.0 ambao hautuamishi maji.

Huhitaji udongo wenye unyevu wa kutosha ili iweze kuota vizuri.

## KALENDA YA KUPANDA ALIZETI

Zao la alizeti hupandwa miezi tofauti kulingana na misimu ya kilimo ya maeneo husika, Kanda ya Kaskazini, Mashariki na Pwani; hupandwa kuanzia mwezi Februari - Machi kulingana na mvua, Kanda ya ziwa: hupandwa kuanzia mwezi Disemba, Nyanda za juu kusini na Kanda ya kati: hupandwa kuanzia mwezi Novemba - Disemba: Kanda ya Magharibi hupandwa kwa misimu miwili mwezi Agosti na mwezi Februari.

Kalenda hii inategemea utabiri wa hali ya hewa na ushauri wa wataalamu wa kilimo waliopo katika maeneo husika.

## MBEGU BORA ZA ALIZETI

Mbegu bora za alizeti zimegawanyika katika makundi mawili kundi la kwanza ni mbegu za chavua huru (OPV) na kundi la pili ni mbegu chotara (hybrid). Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kwa kushirikiana na wakala wa mbegu za serikali (ASA) pamoja na kampuni za mbegu nchini inasambaza mbegu bora za alizeti za chavua huru ambazo ni; Record, TARI-ILO 19 na TARI-NAL 19.

## SIFA ZA MBEGU

| Aina | Kukomaa (siku) | Mavuno | Kiasi cha Mafuta | Rangi ya mbegu | Sifa ya mbegu |
|---|---|---|---|---|---|
| Record | 100 hadi 120 | Magunia 12 hadi 16 ya kilo 60 kwa Ekari | Lita 22 hadi 25 kwa gunia la kilo 60 | Nyeusi yenye mistari midogo ya kijivu | Ina ukizani dhidi ya kuoza vichwa na shina, mabaka ya majani, batobato na kutu ya majani |
| TARI-ILO 19 | 90 hadi 100 | Magunia 12 hadi 18 ya kilo 60 kwa Ekari | Lita 24 kwa gunia la kilo 60 | Nyeusi | Ina ukinzani dhidi ya ugonjwa wa batobato, ubwili unga, mabaka ya majani na kuoza kwa kichwa na shina |
| TARI-NAL 19 | 100 | Magunia 12 hadi 18 ya kilo 60 kwa Ekari | Lita 24 kwa gunia la kilo 60 | Nyeusi | Ina ukinzani dhidi ya kutu ya majani, kuoza kichwa na shina |

## KIASI CHA MBEGU NA NAFASI YA UPANDAJI ALIZETI

Kiasi cha mbegu kinachohitajika kupandwa kwenye eneo la ekari moja ni kilo 2 hadi 3

Panda mbegu 1 au 2 kwa kila shimo kwa nafasi ya sentimita 75 mstari hadi mstari na sentimita 30 shina hadi shina kwa mbegu za (Record na TARI-NAL 19) kwa mbegu ndefu; na sentimita 60 mstari hadi mstari na sentimita 30 shina hadi shina kwa mbegu fupi (TARI-ILO 19). Kina cha shimo la kupandia mbegu kiwe sentimita 2.5 hadi sentimita 5 chini ya udongo ili zipate unyevu wa kutosha na zisiliwe na ndege au wanyama waharibifu

Kwa kutumia nafasi ya kupanda ziliotajwa hapo juu kiasi cha mimea kitakuwa 18,000 hadi 22,000 kwa ekari.



Alizeti iliyopandwa kitaalamu

## MATUMIZI YA MBOLEA

Mbolea za asili (mboji na samadi) na mbolea za viwandani zinaweza kutumika ili kuongeza virutubishi vinavyohitajika kwenye kilimo cha alizeti.

Mbolea yenye virutubishi vya naitrojeni, fosiforasi, potasiam, salfa na boroni zinahitajika kwa uzalishaji wa zao la alizeti.

Kirutubishi cha salfa ni muhimu kwa ajili ya ubora na kiwango cha mafuta na kirutubishi cha boroni ni muhimu katika ukuaji na ujazaji wa punje.

Matumizi ya mbolea yazingatie upimaji wa afya ya udongo au matokeo ya utafiti wa udongo ya eneo husika ili kujua mahitaji halisi ya mbolea.

## UDHIBITI WA VISUMBUFU

Zao la alizeti hushambuliwa na wadudu waharibifu, magonjwa, ndege na wanyama mbalimbali.

Udhibiti wa visumbufu hufanyika kabla na baada ya kupanda kutegemeana na aina ya visumbufu.

Vusumbufu vya magonjwa na wadudu vinaweza kudhibitiwa kwa matumizi ya mbegu bora na kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo.

## PALIZI YA SHAMBA LA ALIZETI

Palizi ifanyike ndani ya wiki 2 - 3 baada ya mbegu kuota. Zoezi hili litaendana na upunguziaji wa miche iliyoota zaidi ya mmoja na kubakiza mmoja wenye afya kwa kila shimo kulingana na nafasi.



Upunguziaji wa miche iliyoota zaidi ya mmoja kwa shimo

## KUVUNA NA KUPURA

Uvunaji wa alizeti kwa wakati hupunguza madhara yatokanayo na wanyama au ndege waharibifu, vichwa kudondoka, kupasuka na kusambaa kwa punje.

Upuraji hufanyika baada ya kuhakikisha kuwa vichwa vya alizeti vimekauka vizuri.



Upuraji wa alizeti baada ya kuvuna

## KUPETA KUKAUSHA NA KUHIFADHI

- Kupeta na kupembua hufanyika ili kuondoa wadudu, mawe, mapepe, punje zilizooza au kupasuka ili kufanya alizeti kuwa ya kichele
- Alizeti inapaswa kukaushwa kwenye jua kabla ya kuhifadhi au kusindikwa ili kufikia kiwango cha unyevu kinachoshauriwa cha asilimia 8.0 hadi 12.
- Alizeti iliyo kaushwa vizuri huhifadhiwa kwenye maghala au vihenge bora vyenye uwezo wa kuzuia uharibifu unaotokana na wadudu, panya, ndege, mvua na unyevu.